# KATIBA YA KIKUNDI
# CHA
# NEEMA

**NO.0721**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO**

***Vikundi vya Kijamii na Kiuchumi***

**CHETI CHA KUTAMBULIWA**

Ninathibitisha kuwa kikundi cha **NEEMA MKONGO** Kutoka Kata ya **MKONGO** ~~Mtaa~~/Kijiji cha **MKONGO NAKAWALE** kimetambuliwa tarehe **16** Mwezi **04** Mwaka **2019** na Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo.

Namba yake ya kutambuliwa ni **NMT/ CBO/0721** Utambuzi huu umetolewa kwa masharti kuwa kikundi hiki kitaendesha shughuli zake katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo na kwa kuzingatia katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na

Katiba ya Kikundi.

Imetolewa leo tarehe ***16*** *mwezi* ***04*** *mwaka* ***2019.***

..................................

***MSAJILI WA CBOs/NGOs (W)***

***NAMTUMBO***

# KATIBA YA KIKUNDI CHA NEEMA.

1. **JINA:** Jina la kikundi litakuwa **NEEMA GROUP.** eneo la shughuli litakuwa Parokia ya Mkongo, ila makao makuu yatakuwa kijiji cha Mkongo Nakawale, kata ya Mkongo, Wilaya ya Namtumbo, makao makuu ya Parokia ya mkongo Jimbo kuu la Songea.

2. **ANUANI:**
Anuani ya kikundi itakuwa S.L.P 682, SONGEA.

3. **MADHUMUNI.**
Kuwaunganisha wanachama na wasio wanachama wa Neema waishio mkongo na waishio nje ya Mkongo katika kuwezesha kuchangia kwa hali na mali, kuendeleza na kusimamia Taasisi za Afya (Zahanati) na Ufundi stadi (Chuo Cha VETA) na kuanzisha miradi mingine ili kuboresha huduma na maisha kwa Wananchi wanaozunguka eneo la Mkongo na nje ya Mkongo.
Kuwajengea uwezo wanakikundi kwa kuwatafutia ujuzi, mafunzo na semina ili waweze kumudu kuendesha shughuli za kikundi na za familia zao kwa ufanisizaidi.

4. **SHUGHULI.**
   - Kuwaendeleza / kuwajengea uwezo wanakikundi kwa utaalamu wa utakaotolewa kwa miradi ya kikundi.
   - Kuhakikisha kila mwanachama anatekeleza vizuri na kwa wakati jukumu atakalopewa na kikundi.
   - Kushirikiana na Bodi ya afya na chuo cha ufundi stadi katika kupanga, kusimamia na kutathmini vipaumbele vya malengo ya mwaka na kuona namna ya kukabili changamoto.
   - Kutafuta vyanzo mbalimbali vya mapato kukidhi lengo la kikundi.
   - Kutafuta utaalamu ili kuboresha na kuwezesha utekelezaji wa lengo.
   - Kutafuta uhusiano na vikundi au vyama mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kupata misaada ya kiufundi na fedha.
   - Kuanzisha miradi mbalimbali ya uwekezaji ili kutunisha mfuko wa kikundi.

5. **UANACHAMA.**
Utakuwa wazi kwa yeyote aliye tayari kuomba, kufuata masharti, katiba na maazimio halali, mwenye sifa zifuatazo:
   a)
   - Awe mwenye akili timamu.
   - Umri usiopungua miaka 18.
   - Mwaminifu na mwadilifu.
   - Mwajibikaji na mtekelezaji wa malengo na wajibu.
   - Kuwa tayari kutoa kiingilio, michango, hisa na michango itakayopangwa na kuthibitishwa na mkutano mkuu.
   - Kuwa tayari kushirikiana na wanakikundi wenzake.
   - Kuwa tayari kujitolea kufanikisha malengo ya kikundi.

5. HAKI ZA MWANACHAMA.

Mwanachama atakuwa na haki zifuatazo:

- Kuwasiliana na viongozi wa kikundi kwaajili ya mambo yanahusu shughuli za kikundi.
- Kupata taarifa ya kikundi kutoka kwa uongozi wa kikundi kuhusu shughuli za kikundi ikiwemo mapato na matumizi ya kikundi.
- Kushirikishwa katika fursa ya kujengewa uwezo pamoja na wanachama wengine.
- Kupata nafasi ya kujieleza ili kujitetea kwa tuhuma yoyote dhidi yake kabla ya uamuzi kutolewa.
- Kutoa taarifa kwa uongozi wake akiona lolote baya kwa kikundi.

6. UKOMO WA UANACHAMA.

Uachama utakaoma kwa;

- Kujitoa kwa hiari au kulazimika.
- Kufukuzwa na mkutano mkuu kwa kukosa sifa au ukorofi.
- Kufa.
- Kuugua maradhi ya muda mrefu yanyozuia utekelezaji malengo.
- Kutohudhuria vikao vitatu mfululizo bila sababu inayokubalika.

NB; Hisa hazitarudishwa kwa mwanachama atakayefukuzwa.

7. UONGOZI.

Kutakuwa na Viongozi katika kikundi;

- Mwenyekiti.
- Makamu mwenyekiti na Naibu makamu mwenyekiti.
- Katibu.
- Katibu msaidizi na katibu mahusiano.
- Mtunza hazina.
- Mwenyekitina katibu wa kamati za miradi yote ya kikundi.

Kamati za miradi zitaundwa ama kufutwa na mkutano mkuu kulingana na shughuli za kikundi.

8. UCHAGUZI.

Kutakuwa na uchaguzi wa viongozi ambao watachaguliwa kwa kura za siri na mkutano mkuu, yaani mkutano wa wanachama wote kila baada ya miaka mitatu(3).
Hata hivyo, unaweza kufanyika uchaguzi mdogowakati wowote kuziba pengo, endapo litakuwapo. Uchaguzi utakuwa huru na wa haki.

9. MUDA WA KUWA MADARAKANI.

- Viongozi watakuwa madarakaini kwa muda wa miaka mitatu.
- Viongozi wanaweza kuwa katika nyadhifa zao si zaidi ya vipindi vitatu mfululizo.
- Baada ya kuwa nje ya madaraka kwa kipindi kimoja , kama mwanachama huyo ataonekana anafaa anaweza kuchaguliwa tena.
- Kiongozi anaweza kusimamishwa na kamati kuu endapo ataonekana kukiuka katiba hii na maazimio halali ya kikundi, au kukiuka maadili ya uongozi, au kutomudu kazi

yake, au akipata ugonjwa unaomfanya asimudu kazi yake kwa muda mrefu, au kupatikana na kosa la Jinai.

- Hata hivyo mkutano mkuu ndio wenye mamlaka ya kumfukuza uongozi.
- Kiongozi anaweza kukoma uongozi wake kwa kujiuzulu kwa barua, kufa, au kuhama eneo la shughuli za kikundi.

## 10. SIFA ZA KIONGOZI.

- Umri usiopungua miaka kumi na nane.
- Upeo mpana na dhamira njema.
- kuwa mfano wa mstari wa mbele katika kutanzua au kutafuta fumbuzi za kudumu za changamoto zinazowakabili watu wote bila kutafuta kwanza faida binafsi.
- Kuwa mfano bora katika uadilifu, uwajibikaji na uaminifu.
- Akili timamu.
- Ufahamu/uwezo wa kutosha kwa nafasi atakayochauliwa.
- Anayeshaurika, kufundishika na kutenda haki.
- Awe tayari /moyo wa kujitolea kufanikisha lengo la kikundi.
- Afahamu vizuri lengo la kikundi an kuwa muumini mzuri wa lengo hilo.
- Kujua vizuri kusoma, kuandika na kuhesabu.
- Ushirikiano naviongozi wenzake na wanachama.

## 11. VIKAO.

### A. mkutano mkuu wa mwaka wa kikundi.

Kutakuwa na mkuu wa mwaka kila mwezi wa kumi *ili kupima* utekelezaji wa malengo ya mwaka na kuwekamalengo ya mwaka unaofuata. Wanakikundi wote ni wajumbe wa mkutano mkuu, hivyo kutakuwa na taarifa ya utekelezaji wa malengo yaliyopita na mapendekezo mapya.taarifa ya mapato na matumizi ni agenda ya lazima katika mkutano huo.

Kila kamati italeta katika mkutano huo taarifa ili mkutano ujiridishe. Mkutano huo unamamlaka ya mwisho. Mwenyekiti atasitisha mkutano, hata hivyo theluthi mbili ya wajumbe wa kamati kuu wanaweza kujiorodhesha na kumwomba mwenyekiti aitishe mkutano ama wanachama waliojiorodhesha wanaweza pia kuomba mkutano mkuu wakati wowote ikiwa kuna jambo la lazima.

### B. Mkutano mkuu wa kawaida.

Mkutano mkuu wa kawaida utafanyika mara moja kila mwezi kujadili mwenendo wa kila siku wa shughuli za kikundi kwa malengo ya mwezi. Wakuu wa kamati wanawajibika kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa malengo mwezi.

### C. Mkutano mkuu maalumu.

Utafanyika wakati wowote kwa jammbo maalumu.

### D. Mkutano wa kamati kuu.

Huu ni mkutano wa viongozi wote kama ilivyoainishwa katika ibara ya saba. Mkutano huu utafanyika kila baada ya mkutano mkuu kuandaa ajenda na mwelekeo wa kikundi. Mkutano huu unaweza kufanyika wakati wowote nje ya wakati kadiri inavyoonekana inafaa.

E. **Kamati tendaji.**

Kutakuwa na mkutano wa kamati tendaji ukiwahusisha viongozi wakuu bila viongozi wa kamati za miradi.

Mkutano huu utakutana mara moja kila mwezi, ikiwepo haja unaweza kukutana zaidi ya mara moja.

F. **Kamati za miradi.**

Kutakuwa na mkutano wa kila kamati mara moja au zaidi kwaajili ya utendaji na kuandaa taarifa za kupeleka mkutano mkuu.

Mikutano yote itaitishwa na mwenyekiti kwa ngazi husika akishirikiana na katibu kwa taarifa isiyopungua siku saba.

12. **AKIDI.**

Katika mikutano ya kikundi akidi itakuwa nusu ya wajumbe, na wajumbe waliotoa taarifa ya udhuru kwa maandishi watahesabika katika akidi.

13. **SHUGHULI ZA KAMATI.**

a. **Kamati kuu**
- Kupokea taarifa za utekelezaji za kamati zote.
- Kutathmini utendaji wa kamati zote.
- Kupokea mapendekezo ya vipaumbele toka kamati zote, kuratibu na kupeleka mkutano mkuu.

b. **Kamati tendaji.**
- Kuongoza, kusimamia, kushauri na kufuatilia utekelezaji wa kamati za miradi.
- Kuhakikisha kikundi kinafikia malengo.
- Kuwajibisha kila anayekwamisha mafanikio kwa kushirikiana na mkutano mkuu
- Kuwakilisha kikundi.
- Kuandaa mkutano mkuu.

c. **Kamati za miradi.**
- Kubuni na kupendekeza mambo ya kufanya,kupanga na kusimamia shughuli za kila siku za kitengo husika.
- Kutoa taarifa ya kila mwezi kwa kamati tendaji kila inapohitajika na kamati tendaji, kamati kuu au mkutano mkuu.
- Kuwajibika na jambo linalohusu kitengo chako.

14. **SHERIA ZA KIKUNDI.**

i. Kila mwanakikundi sharti ajue lengo la kikundi na wajibu wake kadiri ya katiba hii.
ii. Kutekeleza kwa vitendo maamuzi na maazimio ya mkutano mkuu na katiba hii.
iii. Kuhudhuria kila utapotakiwa kwa wakati na bila kukosa.
iv. Kutotenda kinyume na malengo na maazimio ya chama au kikundi.
v. Kupendana wenyewe kwa wenyewe na kupenda shughuli za kikundi.

15. **MALI ZA KIKUNDI.**

- Mali zote za kikundi zitamilikiwa na wanakikundi wenyewe kupitia mkutano mkuu.
- Orodha ya mali za kikundi itakuwa daftari la mali za kikundi na kuhifadhiwa na katibu.
- Mamlaka ya kuuza au kufuta au kutoa mali yoyote ni ya mkutano mkuu wa kikundi.

16. **FEDHA ZA KIKUNDI.**

a. Fedha zote za kikundi zitahifadhiwa Benki au SACCOS na kwahiyo kikundi kitakuwa na akaunti Benki au SACCOS.

b. Wajumbe watatu watakaochaguliwa na mkutano mkuu watatia sahihi Benki na wawili kati yao watatosha kutoa fedha Benki kwa matumizi yaliyopitishwa na mkutano mkuu.

c. Mapato ya fedha za kikundi yatatokana na viingilio vya wanachama, mchango wa kila mwaka, hisa, faida ya miradi ya biashara ya kikundi, ufadhili na michango kama itakavyoamuliwa na kikundi.

17. **USAJILI.**

Kikundi ni lazima kisajiliwe katika ngazi ya Wilaya au Wizara ili kitambulike kisheria.

18. **MSHAURI.**

Ili kupata maoni ya Uma unaotuzunguka, kutakuwa na Mshauri mmoja au wawili wa kikundi kama itakavyo azimiwa na mkutano mkuu, baada ya kupendekezwa na kamati tendaji na kuthibitishwa na mkutano mkuu. Mshauri/Washauri watahudumu katika nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu.

19. **MAREKEBISHO YA KATIBA.**

Marekebisho ya yatafanywa na mkutano mkuu, haja ya kufanya hivyo ikiwepo.

20. **MRITHI.**

Ikitokea mwanakikundi amefariki, hisa za mwanachama aliyefariki zitarithiwa na mwenza wake yaani mke au mume na kama mmoja hana mwenzi, basi watoto wake watarithi. Hata hivyo, ikiwa hakuna mwenzi wala watoto , msimamizi wa mali ya marehemu husika atakuwa ndiye mfuatiliaji wa hisa hizo.

NB: Kwa utekelezaji wa kifungu cha hapo juu, kila mwanachama anatakiwa kuteua mrithi kwa maandishi endapo atataka mrithi tofauti au sawa na maelezo ya hapo juu.

22. **HATI YA KURIDHIA KATIBA.**

Wanachama wa kikundi cha NEEMA tumeridhia katiba hii kuwa `ni halalikwa kikundi chetu kuanzia leo tarehe 17.02.2019.

**ORODHA YA WANACHAMA.**

| NA | JINA | CHEO | JINSIA | NAMBA YA SIMU | SAINI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MOSE E. GUNDA | M/KITI | | 0762847649 | |
| 2 | ELIKANA MABULA | MM/KITI | | 0768300743 | |
| 3 | LEAH F.CHIDAGA | KATIBU | | 0766514446 | |
| 4 | OSMUNDA K.MKINGA | MJUMBE | | 0757723527 | |
| 5 | CHRISTIAN NDINDO | MJUMBE | | 0768229465 | |
| 6 | LOTARD THADEI | MJUMBE | | 0754973171 | |
| 7 | THADEA NTARA | MJUMBE | | 0769849913 | |
| 8 | FEBRONIA NTARA | MJUMBE | | 0762847649 | |
| 9 | ANTONY J.MBALALE | MJUMBE | | 0759531360 | |
| 10 | EUSEBIUS MOYO | MJUMBE | | 0763905773 | |
| 11 | WILSON W. NYAMBO | MJUMBE | | 0765510922 | |
| 12 | DOMINIKUS A.GEHO | MJUMBE | | 0753447241 | |
| 13 | JELOME M.LUAMBANO | MJUMBE | | 0768387350 | |
| 14 | GINSIRA NCHIMBI | MJUMBE | | 0746345749 | |
| 15 | LAURENCIA MVILI | MJUMBE | | 0759875297 | |
| 16 | ALFREDA O.WANDE | MJUMBE | | 0763801095 | |
| 17 | EDITHA MWINGIRA | MJUMBE | | 0759396569 | |
| 18 | SOPHIA NINDI | MJUMBE | | 0769058291 | |
| 19 | ROBERT D.GEHO | MJUMBE | | 0756496740 | |
| 20 | GERVAS A.KAPINGA | MJUMBE | | 0768229468 | |
| 21 | TEODOLA CHALE | MJUMBE | | 0753085690 | |
| 22 | FAUSTA E.MIRINGA | MJUMBE | | 0756823311 | |
| 23 | HELSWIDA MWEGERO | MJUMBE | | 0765510348 | |
| 24 | ASUMTA B.MBILINYI | MJUMBE | | 0769155164 | |
| 25 | ORESTES WANDE | MJUMBE | | 0757835578 | |
| 26 | MENAS D.KAPINGA | MJUMBE | | 0768000064 | |
| 27 | KELVIN W.NYAMBO | MJUMBE | | 0755799507 | |
| 28 | EDINA LWANDA | MJUMBE | | 076456406 | |
| 29 | PASCO E LUAMBANO | MJUMBE | | 0763801748 | |

**Sahihi ya M/kiti** ..........................

**Tarehe** 17-02-2019

**sahihi ya katibu** ..........................

**Tarehe** 17-02-2019

**Katiba ya kikundi na mahudhurio yameshuhudiwa na;**

**Jina** LUKENGELO LAMECK AIDA **sahihi**..........................

**Cheo** HAKIMU MFAWIDHI

**Tarehe** 15-04-2019

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO MKONGO
NAMTUMBO